BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA TATU

Kikao cha Saba – Tarehe 07 Disemba, 2023.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Ripoti ya Saba ya Utekelezaji wa Kazi za Tume ya Maadili kwa Mwaka 2022/2023.

### Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Ripoti ya Saba ya Utekelezaji wa Kazi za Tume ya Maadili kwa Mwaka 2022/2023.

## II. HOJA YA MJUMBE:

### Mhe Asha Abdalla Mussa.

Hoja Binafsi ya Mjumbe kuhusu Kuunga mkono Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020-2025 katika kipindi cha miaka mitatu ya awamu ya nane ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

## III. MASWALI:

### Ofisi ya Rais, Ikulu:

57. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Ikulu:

    Diplomasia ya Uchumi imeleta mchango gani kwa Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi yao.

### Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

22. MHESHIMIWA AZA JANUAR JOSEPH (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

    Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali inaendelea kutekeleza miradi tofauti nchini kwa lengo la kuwaletea wananchi wake maendeleo.

    (a) Ni miradi mingapi hadi sasa tayari imeshapata usajili.

    (b) Ni zipi changamoto ambazo Serikali inakumbana nazo katika usajili huo.

73. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

    Je, ni vikundi vingapi na ni vipi vya watu wenye mahitaji maalum ambavyo vimefanikiwa kupata fedha za mkopo nafuu wa CRDB kupitia mfuko wa uwezeshaji wananchi.

### Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

8. MHESHIMIWA ZAWADI AMOUR NASSOR (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

    Tunaipongeza Serikali kwa kutengeneza na kujenga barabara kuu na za ndani Unguja na Pemba.

    (a) Je, Wizara ina mpango gani wa kuweka taa za barabarani katika eneo la Konde Mjini.

    (b) Kwa kuwa eneo la Konde limekuwa mji kiasi ya kuwa ni

njia kuu ya kuelekea maeneo ya uwekezaji. Je, ni lini barabara hii itawekwa taa kwa maeneo ya mjini.

(c) Kwa kuwa kuwekwa taa za barabarani kunakuza na kuongeza kipato na kuipatia Serikali makusanyo mazuri ya kodi na kunaruhusu biashara kuendelea hadi muda wa usiku, je, ni vigezo gani vinavyotumika katika kuweka taa za barabarani katika maeneo mbali mbali nchini.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

6. MHESHIMIWA ZAWADI AMOUR NASSOR (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa kuwa miongoni mwa kukuza na kuendeleza lugha ya Kishwahili ni kuwepo kwa vitabu vingi vya lugha hiyo vikiwemo vya riwaya, tamthilia, mashairi na vyenginevyo.

(a) Je, ni hatua zipi Wizara itazichukua katika kuboresha maktaba zetu ili zijae vitabu vya Kishwahili vya watunzi mahiri na mashuhuri ambavyo hutumiwa na wasomi wa vyuo.

(b) Je, ni kwa kiasi gani bajeti ya 2023/2024 imezingatia kuondoa changamoto ya kukosekana vitabu katika makataba zetu.

(c) Je, Wizara yako inawashirikisha vipi wataalamu wa maktaba katika ununuzi wa vitabu hivyo.

56. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

(a) Kutokana na uhaba wa madaktari bingwa katika hospitali zetu. Je, wanafunzi wangapi wa fani ya udaktari wamepatiwa udhamini wa masomo hayo katika nchi mbali mbali duniani.

(b) Je, ni yepi matarajio ya Serikali ya kuhakikisha kuwa wanafunzi hao wanarudi nyumbani kuja kutatua tatizo la uhaba wa madaktari kabla hawajaajiriwa katika mataifa mengine duniani.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

36. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA Ameir (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

    Mitaji, masoko na vitendea kazi bora, ni miongoni mwa nyenzo kuu za kuleta ufanisi kwa wavuvi wetu wadogo wadogo kuelekea katika uvuvi wa kisasa na wenye tija.

    Je, ni kwa kiwango gani malengo haya yanawafikia wavuvi wetu hususan wavuvi wadogo wadogo.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

64. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

    Je, Wizara yako ina mpango wowote wa kuendeleza makumbusho ya kuhifadhi viumbe hai kama yalivyoachwa na watawala wa kikoloni.

67. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

    Moja ya sababu za msingi za Zanzibar kukubalika na UNESCO kwa mji wake Mkongwe kuingizwa katika hifadhi ya urithi wa dunia ni kuwepo alama za biashara ya utumwa kwa karne nyingi zilizopita nyuma.

    (a) Je, ni maeneo gani ambayo yanaakisi uwepo wa biashara hiyo maarufu hususan katika karne ya 19 ukitoa soko kuu la biashara ya utumwa liliopo Mkunazini.

    (b) Je, ni kwa kiasi gani maeneo hayo yanahifadhiwa kumbukumbu zake.

    (c) Je, kuna mpango wowote wa kuifufua “slave route” kutoka Tanganyika hadi Zanzibar ikiwa ni sehemu ya vivutio maarufu vya utalii.

**<u>Wizara ya Afya:</u>**

15. MHESHIMIWA ZAWADI AMOUR NASSOR (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

    Tunaipongeza Serikali kwa kuanzisha hospitali za Wilaya na Mikoa.

    (a) Je, Wizara inalifikiria vipi suala la kuanzisha kitengo cha Huduma za Uponaji (Palliative care).

    (b) Je, Wizara ina wataalamu wangapi wa fani hii.

54. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

    (a) Tatizo la maradhi ya ini liko vipi kwa ujumla wake kitathmini.

    (b) Ni nani wanaathirika zaidi kati ya wanawake na wanaume na ni kwa nini.

    (c) Taratibu za matibabu zipo vipi na gharama za matibabu kwa waathirika wa ugonjwa huu wa ini.

**<u>Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:</u>**

78. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

    Nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuanzisha mradi wa ujenzi wa maonesho ya biashara uliopo Nyamanzi.

    Je, ni yepi matarajio ya wajasiramali wadogo wadogo katika kuvuna fursa za mradi huu kabambe.

IV. **HOJA ZA SERIKALI:**

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

Ripoti ya Saba ya Utekelezaji wa Kazi za Tume ya Maadili kwa Mwaka 2022/2023.

V. **HOJA YA MJUMBE:**

**Mhe Asha Abdalla Mussa.**

Hoja Binafsi ya Mjumbe kuhusu Kuunga mkono Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020-2025 katika kipindi cha miaka mitatu ya awamu ya nane ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar

Zanzibar, Raya Issa Msellem
07 Disemba, 2023. KATIBU WA BARAZA.